

HALMASHAURI YA WILAYA YA UKEREWE MKOA WA MWANZA

Phone + 255 0732 - 981174/

Fax + 255 0732 - 981174

Email: Ukerewedc@yahoo.com



Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W),

S.L.P 41,

Nansio – Ukerewe.

15.01.2019

TANGAZO LA ZABUNI.

ZABUNI Na.LGA 092/CTB/2018-2019/02 KWA AJILI YA YA KUFANYA USAFI WA MAZINGIRA NA TOZO ZA FIDIA YA GHARAMA ZA UKUSANYAJI, UZOAJI NA UTUPAJI TAKA.

Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe inatangaza Zabuni kwa watu binafsi, vikundi, kampuni au Mashirika yaliyo na vigezo vinavyostahili kwa ajili ya kutoa huduma ya kufanya usafi wa Mazingira na tozo za fidia ya gharama za ukusanyaji, uzoaji na utupaji wa taka ngumu katika maeneo yafuatayo:-

A: Maeneo ya mji Mdogo wa Nansio, Kata ya kagera, Kata ya kakerege, Kata ya Nkilizya, Kata ya Nakatunguru na Kata ya Bukongo.

B: Maeneo ya Gulio na Soko la Kakukuru, Gulio la bugorola na Gulio la Selema.

MASHARITI MUHIMU:-

1. Muombaji awe na vifaa vya kazi kama inavyoelekezwa katika sheria ya “Usalama mahali pa Kazi”(OSHA)
2. Muombaji awe na Leseni ya Biashara ya huduma ya usafi kutoka Baraza la Afya ya Mazingira na awe na Afisa Afya Mazingira msimamizi.
3. Muombaji awe na watu wa kutosha kusafisha, kukusanya na kutoza tozo za taka katika maeneo ya **kaya, biashara, magulio** na **masoko** katika maeneo yaliyotajwa hapo juu.
4. Muombaji atumie **EFD Mashine** wakati wa kutoza tozo za taka.
5. Idadi ya vikundi/Kampuni vinavyotakiwa ni viwili.
6. Muombaji anashauriwa kutembelea Maeneo yaliyotajwa hapo juu kabla ya kuchukua nyaraka ya Zabuni.
7. Mwombaji awe na uzoefu wa kutosha kuhusu usafi na atoe maelezo jinsi gani atadumisha Usafi na kutunza Mazingira katika eneo analoomba.
8. Njia itakayotumika ni ya Zabuni, Vitabu vya Zabuni vinapatikana Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji(W) **Idara ya Fedha** kuanzia saa **1:30 Asubuhi** hadi saa **9:30 Alasiri** siku za Kazi (**Jumatatu-Ijumaa**) isipokuwa siku za Sikukuu. Vitabu vitapatikana kuanzia **tarehe 16.01.2019 Jumatano.**

9. Malipo kwa ajili ya Ununuzi wa vitabu vya Zabuni ni TSH.50,000/=
10. Vitabu vya Zabuni halisi na Nakala moja vilivyojazwa viandikwe juu ya Bahasha Namba ya Zabuni pamoja na Jina la Zabuni inayoombwa.
Mfano:
Zabuni Na.LGA 092/CTB/2018-19/02 A: Maeneo ya Gulio na Soko la Kakukuru, Gulio la bugorola na Gulio la Selema.
11. Waombaji wote wanatakiwa kuambatanisha vielelezo vyote muhimu vya biashara kwenye Vitabu vyao vya Zabuni, Leseni hai ya Biashara, TIN, Tax clearance Certificate kutoka TRA, Bank statement ya mpaka tarehe 31.12.2018, Company Profile etc.
12. Bahasha ziandikwe kwa "Katibu wa Bodi ya Zabuni, Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe, S.L.P 41, Nansio-Ukerewe" na kisha zitumwe kwa Posta au zipelekwe kwenye sanduku la Zabuni lililopo Makao makuu ya Halmashauri ya Ukerewe, Ofisi ya Katibu Muhtasi wa Mkurugenzi Mtendaji Wilaya kabla ya saa 4:30 (saa nne na nusu) asubuhi tarehe 28.01.2019 siku ya Jumatatu.
13. Ufunguzi wa Zabuni utafanyika tarehe 28.01.2019 siku ya jumatatu baada ya saa 4:30 (saa nne na nusu) asubuhi katika ukumbi mkubwa wa Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe. Waombaji au wawakilishi wao wanakaribishwa kwenye ufunguzi huu.
14. Zabuni itakayochelewa, Zabuni za kielektroniki, Zabuni ambayo haitapokelewa kwa muda na ambayo haitafunguliwa wala kusomwa wakati wa ufunguzi kwa vyovyote vile haitapelekwa katika ngazi ya Tathimini.

Wote mnakaribishwa,

Chaula:
.....

Esther A. Chaula
Mkurugenzi Mtendaji (W)

UKEREWE

MKURUGENZI MTENDAJI (W)
UKEREWE

Nakala kwa:-

- . Mamlaka ya uthibiti wa Ununuzi wa Umma
S.L.P 49,
Dar-es-Salaam.
- . Mkuu wa Wilaya,
S.L.P 2
Ukerewe.
- . Madiwani Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe,
S.L.P 41,
Nansio-Ukerewe.